



رقم: 1446 / 02

التاريخ: 1 Shawwal 1446 H - 30/03/2025 M

بسم الله الرحمن الرحيم

**Hotuba ya Amiri wa Hizb ut Tahrir, Mwanachuoni Mkubwa, Ata Bin Khalil Abu Al-Rashtah kwa Wanaozuru Ukurasa wake kwa Mnasaba wa Idd ul Fitr iliyobarikiwa ya Mwaka 1446 H sawia na 2025 M**  
(Imetafsiriwa)

Sifa njema zote ni za Mwenyezi Mungu, na rehema na amani zimshukie Mtume wa Mwenyezi Mungu, na jamaa zake na maswahaba zake, na wanaomfuata.

Kwa Umma wa Kiislamu, umma bora zaidi kuwahi kuletwala kwa wanadamu:

[كُنْتُمْ خَيْرَ أُمَّةٍ أَخْرَجْتُ لِلنَّاسِ تَأْمِنُونَ بِالْمَغْرُوفِ وَتُشْهِنَ عَنِ الْمُنْكَرِ وَتُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ]

**“Nyinyi mmekuwa bora ya umma walio tolewa watu, kwa kuwa mnaamrisha mema na mnakataza maovu, na mnamuamini Mwenyezi Mungu.”** [Aal-i-Imran: 110].

Kwa wabebaji wa Dawah walio safi na wachamungu, “Na hatumsifu yeyote mbele ya Mwenyezi Mungu,” wanaosema maneno mema na kufanya vitendo vyema. Mwenyezi Mungu (swt) amewasifu wale wenye sifa hizi.

[وَمَنْ أَحْسَنَ قَوْلًا مِّمَّنْ دَعَا إِلَى اللَّهِ وَعَمِلَ صَالِحًا وَقَالَ إِنِّي مِنَ الْمُسْلِمِينَ...]

**“Na ni nani mbora wa kusema kuliko aitaye kwa Mwenyezi Mungu na akatenda mema, na akasema: Hakika mimi ni katika Waislamu?”** [Fussilat: 33].

Kwa watukufu wanaozuru ukurasa wanaoukaribia kwa ukweli na iklasi, na wanaotafuta wema unaowaletea, Mwenyezi Mungu awalipe mema.

Nawapongeza nyote kwa sikukuu njema ya Idd Al-Fitr... na Mwenyezi Mungu (swt) awakubalie amali zenu njema. Hakika Mwenyezi Mungu (swt) huwachunga watu wema.

**Ndugu na Dada Wapendwa:**

Idd hii inakuja na dola ovu ya Kiyahudi inafanya ukatili dhidi ya watu, miti na mawe huko Gaza na Palestina yote, inafanya hivyo kwa msaada wa Marekani, ambayo inaipatia mabomu, makombora na ndege. Ingawa si ajabu kwamba umbile la Kiyahudi kwa kuungwa mkono na Marekani linatekeleza hili, kwani wao ni adui wa Uislamu na Waislamu, lakini cha ajabu ni kwamba hakuna hata mmoja wa watawala katika nchi za Kiislamu anayechukua hatua, hasa wale walioko pambizoni mwa Palestina, ili kuyakusanya majeshi yao kuinusuru Gaza, watu wake, Al-Aqsa, na viunga vyake, na kuling'oa umbile la Kiyahudi kutoka kwenye mizizi yake, na kisha kuiregesha Palestina yote kwa watu wake. Je, yule anayeikalia kwa mabavu ardhi ya Kiislamu na akawatoa watu wake humo hastahiki kupigwa vita na majeshi ya Waislamu na kufukuzwa humo kama walivyowafukuza watu wake?

[وَأَفْلَوْهُمْ حَيْثُ تَقْتَمُو هُمْ وَأَخْرُجُوهُمْ مِّنْ حَيْثُ أَخْرُجُوكُمْ]

**“Na wauweni popote mwakutapo, na muwatoe popote walipo kutoeni,”** [Al-Baqara: 191]. Je, watawala hawatambui hili?! Bali masaibu yao yamewatawala, kwani utiifu wao ni kwa wakoloni makafiri, haswa Marekani, hawakatai amri zake zozote ili kuhifadhi viti vyao vibovu nya utawala.

[فَأَلْتَهُمُ اللَّهُ أَنَّى يُؤْنَكُونَ]

**“Mwenyezi Mungu awaangamizilie mbali! Vipi wanapotoka na haki?”** [Al-Munafiqun: 4]

Basi, kimbiliensi enyi majeshi ya Waislamu kuwanusuru ndugu zenu na dada zenu mjini Gaza, na ikiwa tawala za kidhalimu katika nchi za Kiislamu zitasimama dhidi yenu, basi waondoeni kwa njia zote... na msimamishe utawala wa Mwenyezi Mungu badala yao, Khilafah kwa njia ya Utume, katika kutimiza bishara njema ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw):

«لَمْ تَكُونُ مُلْكًا جَبْرِيَّةً فَتَكُونُ مَا شاءَ اللَّهُ أَنْ تَكُونَ، لَمْ يَرْفَعْهَا إِذَا شاءَ أَنْ يَرْفَعَهَا، لَمْ تَكُونْ خَلَفَةً عَلَى مِنْهَاجِ النَّبِيَّ، لَمْ سَكَتَ

**“Kisha utakuwepo utawala wa kutenza nguvu utakuwepo kwa muda apendao Mwenyezi Mungu uwepo kisha atauondoa apendapo kuuondoa, kisha itakuwepo Khilafah kwa njia ya Utume.’ Kisha akanyamaza (saw).”** [Musnad ya Imam Ahmad]. Kisha Khalifa, wasaidizi wake, na askari wa Uislamu, kutoka daraja la juu hadi la chini kabisa, watatoka kwenye ushindi hadi ushindi, huku wakipiga takbira “Allahu Akbar” na Ummah kupiga takbira “Allahu Akbar” pamoa nao, kwa nguvu na msaada wa Mola wao Mlezi na kujivuna kwa Dini yao, hivyo hakuna adui atakayesubutu kusimamisha umbile katika ardhi ya Uislamu.

[وَيَوْمَئِذٍ يُفْرَحُ الْمُؤْمِنُونَ \* بِنَصْرٍ اللَّهِ يَنْصُرُ مَنْ يَشَاءُ وَهُوَ الْعَزِيزُ الرَّحِيمُ]

**“Na siku hiyo Waumini watafurahi \* Kwa nusura ya Mwenyezi Mungu humnusuru amtakaye. Naye ndiye Mwenye nguvu Mwenye kurehemu.”** [Ar-Rum: 4-5].

Kwa kumalizia, ndugu zangu na dada zangu, nawapongeza sana kwa sikukuu ya Idd al-Fitr, nikimuomba Mwenyezi Mungu (swt) atujaalie kwamba tumetekeleza swala na saumu na qiyam ya mwezi huu mtukufu kwa njia inayomridhisha Mwenyezi Mungu (swt) na Mtume wake (saw). Pia namuomba (swt) kwamba Idd hii iwe mwanzo wa kheri, baraka na utukufu kwa Uislamu na Waislamu.

[وَاللَّهُ عَالِبٌ عَلَىٰ أَمْرِهِ وَلَكِنَّ أَكْثَرَ النَّاسِ لَا يَعْلَمُونَ]

**“Na Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye kushinda katika jambo lake, lakini watu wengi hawajui.”** [Yusuf: 21].

Wassalamu Alaikum Wa Rahmatullah Wa Barakatuh

**Ndugu Yenu**

**Ata Bin Khalil Abu Al-Rashtah**

**1 Shawwal 1446 H Sawia na 30/3/2025 M**